
# IMANI YANGU

HADITHI FUPI



**MWANAWETU MMUNI**

Hakimiliki © Mwanawetu Mmuni

P. O Box 90,

Mtwara - Tanzania

Barua pepe – Mwanammuni@gmail.com

Simu; +255 737966996

ISBN 978-9976-5-7134-9

©2020

Haki zote zimehifadhiwa, hairuhusiwi kuiga, kunakili, kufasiri, kuchapa, au kutoa kitabu hiki kwa njia yeyote ile bila idhini ya Mwandishi.

VITABU VYA MWANAWETU MMUNI TANGU 2017

1. Hasira ni hasara
2. Usimwache atoke “Don’t let him go out” 1
3. Usimwache atoke “Don’t let him go out” 2
4. Usimwache atoke “Don’t let him go out” 3
5. A life after Beijing
6. Jumanne katika msitu wa maajabu
7. Kilimo chetu: Karibu sherehe za Nanenane kitaifa Lindi 2017
8. Come with me
9. Dharau
10. **Imani yangu**
11. Ken na Candy: Shuleni mbali
12. Jifikirie
13. NIFIKIRIE; hii ni hali
14. Nadharia ya maisha ya mti na mtu
15. Falsafa Mtandaoni
16. Safari ya Mikumi
17. Mwenge wa Uhuru na Ukombozi wa Fikra
18. Mzigo wa jirani
19. Unamjua huyu?
20. Hadithi za karne ya 21
21. Elimu mtaani
22. Chumbani
23. Umebadilika

# IMANI YANGU

Katika mji mmoja uliopo pwani ya Bahari ya Hindi kulikuwepo binti mdogo, mrembo sana jina lake Nasma. Alikuwa mstaarabu na Mchamungu, mwenye kufanya ibada na kuvaa mavazi yenye stara.

Wazazi wake walimpenda na kumwamini sana kutokana na tabia yake njema. Hivyo kila alichohitaji, walimpatia wakiamini kinamanufaa pia kumpa faraja kutokana na bidii yake.

Familia hii ilikuwa na watoto wanne. Nasma akiwa mtoto wa pekee kwa kuwa wenzake

walikuwa wakiume na ni mdogo kuliko wote. Kitinda mimba huyo, alichukiwa na ndugu zake sababu waliona upendo wa wazazi wao usiokifani anapewa binti huyo pekee bila ya wao kuhusishwa.

Kaka wa kwanza na nduguye anayemfuata kwa kuzaliwa waliamini mdogo wao anapendwa sababu yeye ni mtoto wa kike na wao wakiume. Walianza kuchukia jinsi yao na kuanza kuwa na tamaa ya kuiga tabia za kike sambamba na kuvaa mavazi yakike. Wakati kaka watatu alipingana na imani ya kaka zake, nae alifikiri upendo wa wazazi wao juu ya Nasma ni kwasababu ya Ucha-Mungu wake. Hivyo kaka huyo


mdogo, alianza kufanya ibada na kutii kikamilifu nguzo zote tano za Uislamu.

Baada ya miaka mingi kupita, watoto wote wanne wa familia hii walikuwa vijana wakubwa. Na walikuwa wanasomea fani mbalimbali katika vyuo tofauti. Ilipofika wakati wa likizo, walirejea nyumbani kuungana na wazazi wao. Nasma na kaka yake mdogo waliendelea kufanya ibada. Kaka zao wakubwa nao pia waliendelea na tabia yakupenda jinsi ya kike na sasa waliokuwa na muonekano unaofanana na wanawake kwa sababu hawakuishia kuvaa mavazi ya kike pekee bali walitumia vipodozi vya kike hivyo kuwa na ngozi nyororo na yakupendeza kama wasichana.

Wazazi wao hawakuwa makini kufuatilia nyendo za watoto wale wasiomcha Mungu. Walijua kila jambo litakalowapata kwa maana ya jema au baya, hayo yatakuwa ni matokeo ya yale waliyoyachagua. Hivyo hawakugundua mabadiliko ya matendo yao yaliyokinyume na jinsi yao.

Mara nyingi Nasma alipenda kuswali Swalah ya Jamaa. Siku moja akiwa anaelekea msikitini kwa ajili ya ibada ya Magharibi alikutana na Bibi kizee mmoja. Baada ya kumsalimia, Bibi kizee alijitambulisha kuwa ni mgeni katika mji huo pia macho yake yanauono hafifu, hivyo anaomba msaada wa kupelekwa msikitini.

Nasma alisita kidogo! Lakini alikubali na wakaelekea huko pamoja.



Walipofika msikitini; Bibi kizee na Nasma walichukua udhu kisha kuingia ndani

kuswali. Mwisho wa ibada Bibi kizee hakumuona Nasma hivyo aliondoka peke yake kuendelea na safari yake.

Usiku huo Nasma alipatwa na homa kali. Wazazi wake walimpeleka hospitali ili kupata matibabu. Baada ya vipimo, Nasma hakugundulika kuwa na maambukizi yoyote ya ugonjwa wowote. Mwili wake ulionekana hauna shida yoyote hivyo alipewa huduma ya kwanza ili kumwezesha kupata fahamu halafu waliruhusiwa kurudi nae nyumbani.

Nasma aliugua kwa muda mrefu. Wazazi wake waliwaalika wanavisomo mbalimbali ili kumwombea rehema za Mola mgonjwa wao aweze kupona lakini kwa bahati mbaya

hata nafuu haikupatikana. Miezi ilikwenda hadi ikawa mwaka kisha miaka.

Kaka zake Nasma walimaliza masomo na kuajiriwa. Kaka mkubwa na ndugu yake walifurahia hali iliyomtokea dada yao kwa kuwa waliamini itaondoa kisirani cha wazazi wao juu yao kwa kuwa wao wameshamkufuru Mungu. Lakini kaka mdogo aliendelea kumuomba Mwenyezi-Mungu kutoa msamaha kwa ndugu zake pamoja na wazazi wake.

Mara kwa mara aliomba ruhusa kazini kwake ili afanye safari ya kwenda kuwajulia hali wazazi wake pamoja na ndugu yake Nasma.

Baada ya safari ndefu, alisikia Adhana akiwa umbali wa mita chache tu kufika nyumbani kwao. Aliamua kwenda msikitini kuswali kwanza kabla ya kufika nyumbani kwao kwakuwa muda wa ibada ulikuwa umeshafika. Aliiacha gari yake na kutembea kwa miguu kuelekea msikitini. Njiani alikutana na Bibi kizee ambaye alikutana na Nasma miaka kadhaa iliyopita kabla ya kupata maradhi. Bila kujua, alikubali kumpeleka msikitini na alimwambia;

“Ambatana nami, sababu ninaelekea huko huko.”

Baada ya ibada, Bibi kizee alitoka nje ya msikiti na kumkuta kaka yake Nasma anamsubiri.

“Nilijua umeshaondoka.” Alisema bibi kizee.

“Ninakumbuka uliniambia u mgeni katika mji huu. Nilikuwa ninawahi ibada, sikuweza kukuhoji zaidi kama ulihitaji msaada mwingine toka kwangu.” Alijibu kaka yake Nasma.

“Ah, wewe ni mkarimu sana. Asante!”

Waliendelea na maongezi wakiwa wanaelekea nyumbani kwa wazazi wake baada ya kumuomba mgeni huyo apate chakula cha usiku na kupumzika ili siku ya pili aendelee na safari yake.

Bibi kizee alijieleza kuwa ni msafiri. Anakwenda kutembelea familia yake iliyopo kilometa mia sita kutoka mji huo. Hivyo siku ya pili atapata usafari wakumfikisha mji huo.

Wazazi waliwapokea kwa furaha. Baada ya utambulisho, wazazi wa Nasma walimuomba Bibi kizee wampe hifadhi ya malazi katika nyumba yao badala ya mpango wake wakwenda kulala hotelini. Nae bila hiyana, alikubali.

Kaka alikwenda chumbani kwa dada yake kumjulia hali ndugu yake. Nasma hukaa chumbani kwake siku mzima isipokuwa muda wa chakula cha usiku ndipo anawekwa kwenye kiti cha magurudumu na

kwenda sebuleni kupata chakula akijumuika na familia. Walifanya hivyo ili kumpa upendo na kumfariji wasionekane wanamtenga kutokana na maradhi aliyoyapata.

Muda wa chakula ukafika, Nasma aliletwa mesini kama ilivyo desturi yao. Alipofika tu na kukutana uso kwa uso na Bibi kizee, Nasma alianza kutetemeka na kuporomoka toka kwenye kiti hadi chini kama furushi kisha kusota kama nyoka kuelekea alipokaa Bibi kizee. Alipomfikia alianza kulia na kuomba msamaha akimshika miguu. Ilistaajabisha sana kwakuwa ni miaka mingi haijasikika sauti ya binti huyo pia sababu ya

Nasma kuomba msamaha kwa mgeni asiyemfahamu.

Bibi kizee alikubali kutoa msamaha kwa sharti la Nasma kusema ukweli wa uovu wake na kutubu kwa Muumba wake. Kusikia vile, kaka yake alimsihi dada yake kukubali sharti hilo na kumuahidi kushirikiana nae bila kumtenga. Sababu ndiyo kazi aliyokuwa anaifanya katika ibada zake. Aliomba utukufu wa Mungu uwaangazie ndugu zake waweze kuzishinda anasa za dunia na kufuata miongozo ya dini kwa kumcha Mungu. Nasma alipata nguvu ya kukaa kitako na kusema;

“Wazazi wangu na kaka yangu, ninaomba mnisamehe kwa makosa niliyoyafanya. Niliwadanganya ninyi wazazi wangu, walimwengu pamoja na nafsi yangu. Nilitumia uaminifu mlionipa kufanya matendo yasiyomridhisha Mungu wala kupendeza machoni pa watu.” Alisita kuendelea kuongea.

Watu wote walishtuka isipokuwa Bibi kizee. Nasma alimwangalia Bibi huyo kwa jicho la huzuni ili apewe msamaha na ikiwezekana kuponywa bila kutoboa siri yake mbele ya kadamnasi. Lakini macho ya Bibi kizee yalianza kubadilika na kutoa mwanga mkali na watu wote walianza kuogopa sababu walitambua kuwa bibi huyo hakuwa mtu wa

kawaida. Kaka yake alimfuata Nasma na kumwambia;

“Hakuna siri ya binadamu mbele ya Mwenyezi Mungu. Ulishindwa kuitunza siri yako, Bibi kizee akaijua hivyo ni heri useme ukweli na kutubu kwa Mola wetu. Nae ni mwenye rehema, atakusamehe.” Baada ya maneno haya, Nasma alifuta machozi na kukohoa kidogo kulainisha koo halafu akaendelea.

“Siku niliyopata maradhi niliaga kwenda msikitini kuswali swala ya Magharibi lakini sikuwa nimetia nia ya kwenda kwenye ibada hiyo bali nilikusudia kwenda kukutana na rafiki yangu wa kiume. Ilikuwa ni desturi yetu kukutana muda huo, ndiyo sababu

nilikuwa sipendezwi kuswali nyumbani. Tulipofika msikitini nilisimama msitari wa nyuma wenye watu wachache ili niweze kutoroka bila kuleta usumbufu kwa waumini."

Alianza kulia tena na kuomba msamaha. Baba Nasma alipandwa na jazba na kumrukia alipokaa na kuanza kumkaba koromeo. Kaka yake Nasma alimpapatua baba yake shingoni mwa Nasma kisha alimtuliza. Mama Nasma alishikwa na bumbuwazi na kuishia kutumbua macho bila kutoa sauti wala kutikisika ingawa alionesha kutamani kufanya kitu.

"Nilifanikiwa kufika kwa bwana wangu, na baada ya stori nilirejea nyumbani

nikiambatana nae. Njiani tulikutana nae tena ……! (alimuonesha Bibi kizee) Pale pale sikujua kilichoendelea, ninashangaa ninamuona tena hapa nyumbani. Ninajuta kwa kufanya kufuru hiyo, naomba msamaha kwa Mungu wangu pamoja nanyi wazazi wangu pia. Poleni kwa kwenda kinyume na yale mliyoyatarajia toka kwangu. Asante kaka yangu kwa kuniokoa kwenye shimo la jehanamu nilikokuwa ninaelekea. Naomba msamaha Bibi kizee, nilikudanganya na kukutoroka nikiwa ninajua nilikuwa msaada kwako…!”

Kabla watu wote hawajatoa neno kutokana na maelezo ya siri yaliyotolewa na Nasma, mlango uligongwa na kufunguliwa kwa

haraka na kuingia kaka wa pili akiwa anahema kavalia mavazi na urembo uliozidisha mshangao. Alivaa kaptura yakubana mwili, fulana, kidani, pete mbili, na vikuku kwenye miguu yote miwili.

Alipofika ndani alianza kulia na kutoa taarifa ya kifo cha kaka yake mkubwa aliyepigwa risasi baada ya kutaka kuwakimbia Polisi. Alieleza kuwa wanajihusisha na mambo ya ushoga na matumizi ya dawa za kulevya. Siku ya tukio, kaka yake alisafiri kwenda kwenye nchi yenye sheria kali juu ya masuala ya ushoga. Kwa kuwa anatumia dawa za kulevya, ilimfanya kutojali chochote na kuvunja sheria za nchi hiyo. Baada ya purukushani za kujiokoa kwenda

jela askari mmoja alimfyatulia risasi na kufariki papo hapo. Baada ya uchunguzi wa awali alikutwa na madawa ya kulevya ambayo aliyahifadhi kwenye viatu vyake.

“Nilipata taarifa toka kwa rafiki zake. Hivyo mwili upo kwenye chumba cha kuhifadhia maiti. Naomba mnisamehe sana na msamehe na kaka pia. Tuliamua kuingia katika shughuli hiyo baada ya kuona ninyi wazazi wetu mmeelekeza upendo wenu kwa dada Nasma pekee. Tulijua mnachokipenda ni jinsi yake, hivyo nasisi tuliamini mtoto wakike ana thamani kwa wazazi na jamii kuliko mtoto wa kiume. Hivyo tulianza kujibadilisha kuwa wanawake. Tulishindwa kufanya upasuaji

kwa kuwa hatukuwa na fedha za kulipia gharama. Hivyo tuliendelea kutafuta fedha kwa udi na uvumba hadi pale mimi nilipochukua fedha za karo zetu. Nilifanikiwa kufanyiwa upasuaji na hapa nilipo nimeolewa!”

Kusikia vile, wazazi wote wawili walizimia na Bibi kizee aliyeyuka na kuondoka kwa kishindo cha upepo. Watoto waliwasaidia wazazi wao waweze kupata fahamu. Baada ya juhudi kubwa, baba yao alipata fahamu na kubakia mama yao. Walimchukua na kumpeleka hospitali haraka. Wakati huo Nasma alikuwa amepona kabisa.

Madaktari walitia bidii kubwa kuokoa maisha ya mama Nasma lakini ilishindikana

na ilipofika siku ya pili alikata roho. Kuona vile kaka wa pili nae alikunywa sumu hivyo kukawa na misiba mitatu katika nyumba moja.

Ili kuokoa maisha ya waliobaki, kaka mdogo aliomba muda wa kuwaelimisha wanafamilia juu ya elimu ya uwepo wa Mungu na uweza wake katika maisha ya binadamu. Hivyo yawapasa kumcha Mungu kwasababu hakuna kiumbe wala kitu chenye haki ya kuabudiwa zaidi ya Mungu mmoja.

*MWISHO.*